



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 21/10/2021

**TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA YA KAZI ZA UFUNDI KWA AJILI YA UJENZI
WA VYUMBA 55 VYA MADARASA**

ZABUNI NA. LGA/071/2021/2022/RDC/W/25 LOT 1-18

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO -19.
2. Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya inakaribisha kazi za Mikataba ya Muda Mfupi za Mafundi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za Ujenzi wa Miundo mbinu ya Serikali kwa ajili ya Ujenzi kwa njia ya Manunuzi ya "Force Account" katika fani zifuatazo:-
 - i. Fundi Uashi (ambao utajumuisha pia upakaji wa rangi na Ufundi umeme)
 - ii. Fundi Aluminium (Utengenezaji wa madirisha)
 - iii. Fundi Seremala (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).

Sifa za muombaji

- i. Awe Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
- ii. Awe na Namba ya Utambulisho wa Ulipaji Kodi (TIN)
- iii. Awe na akaunti kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe
- iv. Awe na ujuzi wa kusoma ramani na kuelezea.
- v. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi za serikali na mwenye uelewa na taratibu zake. Aambatanishe nyaraka muhimu ili kuthibitisha uzoefu wake katika kufanya kazi za Serikali (yaani aambatanishe nakala za barua za tuzo za kazi alizowahi kufanya, nakala za mikataba ya kazi za ujenzi, nakala za Hati za Malipo za kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2021).

- vi. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha (Mtaji) wa kuwalipa mafundi wake wasaidizi pasipo kuomba kulipwa malipo ya awali (Advance Payments); na kwa msingi huo aambatanishe na taarifa za kibenki (Bank Statement) angalau ya mwaka mmoja (1).
- vii. Awe mzalendo na mwenye kujituma katika kazi.
- viii. Awe na Elimu angalau cheti cha ufundi

3. Miradi ya ujenzi wa madarasa inatarajiwa kufanyika katika Shule za Sekondari zifuatazo:-

KITALU NA.	JINA LA SHULE	IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA
1.	Ziwa Ngosi	3
2.	Nkunga	1
3.	Ndanto	4
4.	Mpuguso	2
5.	Masukulu	2
6.	Kalengo	2
7.	Ndembela One	3
8.	Kyimo	2
9.	Ukukwe	2
10.	Mpandapanda	3
11.	Kiwira	3
12.	Kinyala	6
13.	Itagata	4
14.	Iponjola	3
15.	Kayuki	4
16.	Ikuti	3
17.	Bulyaga	4
18.	Bujinga	4

Aidha, Mwombaji anapaswa kuzingatia masharti yafuatayo:-

- a) Mwombaji lazima aandike barua ya maombi kwa jina lake binafsi au kwa jina la biashara akiainisha mradi anaokusudia kujenga.
- b) Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.
- c) Mafundi watakaobahatika kupata kazi watalazimika kuajiri mafundi wasiopungua 2 wenye uwezo na uzoefu, wasaidizi wa kutosha kwa kadri ya ukubwa wa kazi husika.
- d) Awe tayari kufanya kazi muda wote hadi hapo mradi utakapokamilika bila visingizio.

4. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu katika upande wa sifa na masharti ziwawasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmshauri ya Wilaya ya Rungwe, S.L.P 148, Tukuyu yakiwa yamefungwa vizuri kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la mradi unaoombwa.
5. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi tajwa hapo juu ni tarehe 25/10/2021 saa 9:30 Alasiri. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya hapo hayatakubaliwa.
6. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi/kampuni utakaofanyika tarehe 26/10/2021 saa 4:00 asubuhi tafadhali zingatieni muda huu.
7. Wako katika Ujenzi wa Taifa,



Mchau, R.B

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE